

RIPOTI YA EMISSIONS GAP MWAKA WA 2022, UJUMBE MUHIMU

RIPOTI YA EMISSIONS GAP MWAKA WA 2022: Kupunguza Pengo-hatua duni za kushughulikia mazingira zinapelekea hitaji la mabadiliko ya dharura kuwa chaguo la pekee.

Kadiri athari mbaya kwa hali ya hewa zinavyozidi kuongezeka, [*Ripoti ya Emissions Gap Mwaka wa 2022: Kupunguza Pengo – Changamoto za mazingira zinapaswa kushughulikiwa kwa dharura katika jamii*](#) inaonyesha kuwa dunia bado kufikia malengo ya mazingira katika Mkataba wa Paris, na inakosa mikakati ya kuaminika ya kufikia nyuzijoto 1.5. Ni mabadiliko ya dharura tu ya mfumo mzima ndiyo yatakayoweza kuzuia changamoto za mazingira zinazoongezeka. Ripoti hii inaangazia jinsi ya kuleta mabadiliko haya, kupitia hatua katika sekta ya usambazaji wa umeme, viwanda, uchukuzi na ujenzi, na kupitia mifumo ya chakula na ya kifedha.

Licha ya wito wa kuimarishwa kwa Ahadi Zinazotolewa na Taifa (NDCs) kufikia mwaka wa 2030, hatua zinazopigwa tangu kutokea kwa COP26 mjini Glasgow bado ni duni zaidi.

- NDC zilizowasilishwa tangu COP26 ilipotokea hupunguza tu kiwango cha gigatoni 0.5 cha uzalishaji wa gesi yakaboniksidi (GtCO₂e), chini ya asilimia moja, kuzingatia makadirio ya uzalishaji wa gesi chafu duniani kufikia mwaka wa 2030.
- Kwa kuzingatia NDC zote mpya na zilizosasishwa zilizowasilishwa kati ya tarehe 1 Januari mwaka wa 2020 na tarehe 23 Septemba mwaka wa 2022, ni idadi ya mataifa 166, yanayowakilisha asilimia 91 ya uzalishaji wa gesi ya ukaa, ongezeko kutoka kwa mataifa 152 kufikia wakati wa COP26.
- Wanachama wengi wa G20 ndio wameanza kutekeleza juhudi za kufikia malengo yao mapya; kwa ujumla, G20 inatarajiwa kushindwa kutimiza ahadi zake za mwaka wa 2030 isipoimarisha juhudi.

Ukosefu huu wa kupiga hatua unafanya dunia kuendelea kushuhudia ongezeko la joto zaidi ya lengo la Mkataba wa Paris la chini ya nyuzijoto 2, na ikiwezekana nyuzijoto 1.5.

- NDC zinazotolewa kwa hiari zinakadiriwa kutoa fursa ya asilimia 66 ya kudhibiti ongezeko la joto duniani lisizidi takriban nyuzijoto 2.6 kufikia mwishoni mwa karne hii. Kwa NDC zinazotolewa kwa masharti, kiwango hiki kitashuka hadi nyuzijoto 2.4.
- Sera zilizopo kwa sasa, zisipoimarishwa zaidi, zinakadiriwa ongezeko la nyuzijoto 2.8.
- Utekelezaji wa NDC zote pamoja na ahadi za kutozalisha hewa chafu zilizotolewa na idadi inayoongezeka ya nchi zinaonyesha kuna ongezeko la nyuzijoto 1.8. Hata hivyo, hali hii si ya

kuaminika, kwa kuzingatia tofauti kati ya uzalishaji wa hewa chafu kwa sasa, malengo ya hivi karibuni ya NDC na malengo ya kudumu ya kutozalisha hewa chafu.

Ili kuweza kufikia malengo ya Mkataba wa Paris, ulimwengu unapaswa kupunguza gesi ya ukaa kwa kiwango kikubwa katika kipindi cha miaka minane ijayo.

- NDC zinazotolewa kwa hiari na zile zinazotolewa kwa masharti zinakadiriwa kupunguza uzalishaji wa hewa chafu duniani kufikia mwaka wa 2030 kwa asilimia 5 na 10 mtawalia, ikilinganishwa na uzalishaji wa gesi chafu kwa kuzingatia sera zilizopo kwa sasa.
- Ili kuwa na njia nafuu ya kupunguza ongezeko la joto duniani lisizidi nyuzijoto 2 na nyuzijoto 1.5, ni sharti asilimia hizi zifike asilimia 30 na asilimia 45 mtawalia.
- Uzalishaji wa gesi chafu sharti uendelee kupungua kwa kasi baada ya mwaka wa 2030 ili kuepuka kumaliza bajeti ya gesi ya ukaa iliyosalia.

Upunguzaji huo mkubwa unahitaji mabadiliko makubwa, ya kasi na ya kimfumo kote ulimwenguni.

- Ripoti inaangazia hatua zinazohitajika katika sekta ya usambazaji wa umeme, viwanda, uchukuzi na ujenzi, na katika mifumo ya chakula na ya kifedha ambayo itasaidia mabadiliko haya.
- Hata kama mabadiliko haya hayatafanikiwa kuziba kikamilifu pengo la uzalishaji wa hewa chafu kufikia mwaka wa 2030, kila kipande cha digrii ni muhimu. Kuzindua mabadiliko ni muhimu ili kuwezesha kuwa na mustakabali usio na hewa ya ukaa utakaotwezesha kudhibiti ongezeko la joto duniani na kutoa manufaa mengine ya jamii na kwa mazingira, kama vile hewa safi, ajira isiyochafua mazingira na upatikanaji wa nishati kwa wote.

Mabadiliko ya kuwezesha kutozalisha gesi ya ukaa katika usambazaji wa umeme, viwandani, kwenye sekta ya uchukuzi na ujenzi yanaendelea lakini yanahitaji kuimarishwa.

- Usambazaji wa umeme umeendelea zaidi, kwa sababu gharama za nishati jadidifu kutoka kwa jua na upepo zimepungua, lakini bado kuna changamoto - ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mabadiliko ya haki na upatikanaji wa nishati kwa wote.
- Kwa majengo, teknolojia zilizopo kwa sasa zinahitaji kutumika kikamilifu. Kwa viwanda na uchukuzi, teknolojia ya kutozalisha hewa ya ukaa inapaswa kuendelea kukuzwa na kutumiwa zaidi.
- Mwongozo wa hatua muhimu za kuimarisha mabadiliko ni pamoja na:
 - kuepuka kutumia miundomsingi mipya inayotumia mafuta mengi ya visukuku,
 - kukuza zaidi teknolojia isiyozalisha hewa ya ukaa, miundo ya soko na mipango inayoleta mabadiliko ya haki,
 - kutumia teknolojia ya kutozalisha hewa chafu na mabadiliko ya kimienendo ili kudumisha upunguzaji hadi kutozalisha kabisa hewa ya ukaa.

Mifumo ya chakula, ambayo hukadiriya theluthi moja ya uzalishaji wote wa hewa chafu, inaweza kubadilishwa ili kuwa upunguzaji wa haraka na wa kudumu.

- Maeneo ya kuzingatia kwa mifumo ya chakula ni pamoja na mabadiliko ya lishe yanayohitajika (ikiwa ni pamoja na kukabiliana na uharibifu wa chakula), kutunza mifumo asilia ya ekolojia, uboreshaji wa uzalishaji wa chakula shambani na uondoaji wa hewa ya ukaa kwenye mifumo ya usambazaji wa chakula.
- Mabadiliko katika maeneo haya manne yanaweza kupunguza uzalishaji wa hewa chafu wa mifumo ya chakula kufikia mwaka wa 2050 kwa takribani theluthi moja ya viwango vya sasa; kinyume na uzalishaji wa hewa chafu unaoongezeka karibu maradufu iwapo hali ya sasa itasalia ilivyo.

- Serikali zinaweza kuleta mabadiliko kwa kufanyia marekebisho ruzuku na mifumo ya ushuru. Sekta ya kibinafsi inaweza kupunguza ubathirifu na uharibifu wa chakula, kutumia nishati jadidifu na kukuza vyakula vipya vinavyopunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa. Kila raia anaweza kubadilisha mtindo wake wa maisha ili kutumia chakula kinachopelekea mazingira endelevu na kupunguza hewa ya ukaa.

Mfumo wa kifedha ni sharti ukabiliane na changamoto za ndani na nje ili kuwa mstari mbele kuleta mabadiliko katika sekta mbalimbali.

- Mabadiliko ya kimataifa ya kuwa na uchumi wa kiwango cha chini cha hewa ya ukaa yanatarajiwa kuhitaji uwekezaji wa angalau Dola za Marekani kati ya trilioni 4 na 6 kwa mwaka. Hii ni sehemu ndogo tu (asilimia kati ya 1.5 na 2) ya jumla ya mali ya sekta ya fedha inayosimaniwa, lakini muhimu (asilimia kati ya 20 na 28) kuzingatia rasilimali za ziada za kila mwaka zinazohitajika.
- Utoaji wa fedha hizo utahitaji mabadiliko ya mfumo wa fedha na miundo na taratibu zake, kushirikisha serikali, benki kuu, benki za biashara, wawekezaji wa taasisi na wahusika wengine wanaotoa ufadhili.
- Mbinu sita za mabadiliko hayohohitajika kwenye sekta ya fedha, ambayo ni lazima yafanywe kwa njia ijumuishi, ni:
 - **Kuimarisha zaidi masoko ya fedha**, ikiwa ni pamoja na kupitia kwa uainishaji na uwazi.
 - **Kuanzisha kuwekea bei hewa ya ukaa**, kama vile ushuru au mifumo ya biashara.
 - **Kuchunguza matumizi ya fedha**, kupitia kuhamasisha umma kuhusu sera, ushuru, matumizi na kanuni za kutumia fedha.
 - **Kubuni masoko ya teknolojia ya kiwango cha chini cha hewa ya ukaa**, kupitia kubadilisha mzunguko wa fedha, kuchochea uvumbuzi na kusaidia kuweka viwango.
 - **Kuhamasisha benki kuu**: benki kuu zinazidi kushughulikia changamoto za mazingira, ila hatua madhubuti zaidi kuhusu sheria zinahitajika kwa dharura.
 - **Kuanzisha "vilabu" vya mazingira katika nchi zitakazokubali, kuanzisha miradi ya kifedha katika nchi mbalimbali na ubia kupitia mabadiliko ya haki**, ambayo yanaweza kubadilisha kanuni za sera na kubadilisha mkondo wa fedha kupitia vifaa vya kifedha vya kuaminika, kama vile dhamana huru.